JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

616 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

Muda: Saa 3 Hours **Mwaka: 2024**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza hatua nne za kufuata katika kuandaa mpango kazi.
2. Pendekeza hatua za kuchukua ili Waislamu waepuke tabia na mambo ya kizinifu.
3. Eleza vigezo vinavyoitofautisha Qur'an na vitabu vingine vya Mwenyezi Mungu (S.W).
4. Fafanua kwa kifupi mbinu nne za ulinganiaji alizotumia Nabii Nuhu (A.S) na wanazotumia walinganiaji wa leo.
5. Bainisha kwa kifupi hoja nne kupinga mgawanyo potofu wa elimu unaosambazwa na baadhi ya Waislamu.
6. Bainisha hoja nne zinazoonesha umuhimu wa Sunnah katika maisha ya kila siku.
7. Tumia hoja nne kueleza kwa ufupi hatua za kufuata katika kumshonea sanda maiti wa kiume.
8. Eleza kwa ufupi hatua nne za kufuata katika ufundishaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu darasani.
9. Tumia hoja nne kueleza matokeo au ujuzi atakaopata mwanafunzi wa shule ya msingi baada ya kujifunza somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.
10. Eleza kwa ufupi mikakati minne atakayofanya mwalimu ili kumwezesha mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi.

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Tumia hoja tano kufafanua mchango wa Uislamu na Waislamu katika kupigania uhuru wa Tanganyika.
12. Tumia hoja sita kuthibitisha faida za kuufuata Uislamu katika maisha ya kila siku.
13. Chambua mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini.
14. Eleza mambo sita ya kuzingatia wakati wa kutumia ubao katika ufundishaji yanayoonesha usanaa na usayansi.